**St. Thomas Institute of Management and Technology**
(Songea Campus - Fully Accredited, Reg. No. NACTE/BTP/008; Msata Campus Reg. No. NACTE/BTP/092P)
Airport Road, Ruhuwiko, P. O. Box 998, SONGEA
Pugini area, Msata Township, P. O. Box 163, CHALINZE
chagua@stimat.ac.tz, www.stimat.ac.tz
Tel: 0767778069, 0622818818, 0765914576, 0717710468, 0763409901

Kwa:

____________________________________

____________________________________

**YAH: FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA ASTASHAHADA (CHETI) AU STASHAHADA (DIPLOMA)**

Fomu hii ni maelekezo kwa ajili ya wenye sifa kujiunga na chetu cha St. Thomas Institute of Management and Technology (STIMAT) kilichopo Ruhuwiko Songea Mjini pembezoni mwa barabara iendayo Uwanja wa Ndege wa Songea (mkoa wa Ruvuma). Fomu hii inawahusu wanafunzi wenye sifa ya:

(i) Kujiunga na kozi ngazi ya Cheti au Diploma; na
(ii) Kuhamia katika kozi ngazi ya Cheti au Diploma;

Chuo cha St. Thomas Institute of Management and Technology (SONGEA) kilianzishwa mwaka 2013 na kupata Usajili Kamili (Full Registration) chini ya NACTE wenye nambari NACTE/BTP/008. Hivi sasa chuo chetu ni moja ya vyuo vyenye ITHIBATI (Accreditation) ya Baraza (NACTE) kuanzia Desemba 2017.

## 1. UTANGULIZI

Jaza fomu hii na kuja nayo chuoni ikiwa na risiti ya malipo ya awali ili kujiunga na mojawapo ya kozi zinazotolewa na **St. Thomas Institute of Management and Technology.** Malipo yafanyike. benki ya *CRDB Akaunti Na. 0150245471600*, Jina la Akaunti St. Thomas Institute of Management and Technology. Taarifa zako zitatuwezesha kukamilisha udahili na kuhakiki sifa zako kwenye mfumo wa *NACTE.*

| Na. | Kozi | |
|---|---|---|
| 1. | Maendeleo ya Jamii (Community Development) | ( ) |
| 2. | Utunzaji wa Nyaraka, Kumbukumbu na Habari (Records, Archives and Information Management) | ( ) |
| 3. | Elimu ya Biashara (Business Administration) | ( ) |
| 4. | Kompyuta, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Computing, Information and Communication Technology) | ( ) |
| 5. | Ustawi wa Jamii (Social Work) | ( ) |
| 6. | Kilimo (General Agriculture) | ( ) |
| 7. | Nursery Teaching (Ualimu wa Watoto Wadogo) | ( ) |

Nafasi hii itakuwezesha kupata AJIRA na na pia kujiunga na mafunzo ya juu katika vyuo vilivyo chini ya Baraza (NACTE) na pia vyuo vikuu (TCU).

## 2. MAELEZO MUHIMU YA KUJIUNGA NA CHUO

Kujiunga na chuo chetu kunaambatana na sharti la kuwa na sifa stahiki za kujiunga na program/kozi husika. Kwa wale ambao wana sifa pungufu, chuo kinatoa nafasi za kurudia mitihani kupitia sekondari yake ya Taifa Foundation inayotoa mafunzo bure kwa wanachuo wa STIMAT na mtahiniwa atatakiwa kulipia gharama za usajili na mitihani hiyo tu. Chuo pia kinapokea wanafunzi waliofuzu mafunzo kutoka vyuo vingine na wanaohamia. Wanafunzi hawa wanaweza kujiunga na ngazi za juu zitolewazo hapa chuoni yaani NTA Level 5 (Cheti) na NTA Level 6 (Diploma).

## 3. USAJILI NA KUANZA MASOMO

Masomo yataanza 5 Machi 2019 na iwapo utashindwa kuripoti kwa sababu yoyote ile unashauriwa kuwasiliana na Menejimenti ya Chuo kwa namba za simu 0767778069 au 0754686669 au 0622818818 au 0736818818 au 0717710468 andika baruapepe chagua@stimat.ac.tz au principal@stimat.ac.tz.

## 4. SIFA ZA KUJIUNGA NA KOZI MBALIMBALI

Sifa za kujiunga kama zilivyoidhinishwa na Baraza (NACTE) ni kama ifuatavyo:

| Programu/Kozi | Ngazi ya Mafunzo | Sifa za Kujiunga |
|---|---|---|
| Maendeleo ya Jamii (Community Development)<br><br>Utunzaji, Kumbukumbu, Nyaraka na Habari (Records, Archives and Information Management)<br><br>Biashara (Business Administration)<br><br>Ustawi wa Jamii (Social Work)<br><br>(Kompyuta, Habari na Teknolojia ya Mawasiliano (Computing, Information & Communication Technology) | (Basic Technician Certificate) NTA Level 4 | Ufaulu wa pasi ya D kwa masomo yoyote manne (4) ya kidato cha nne<br>au<br>cheti cha VETA NVA ngazi ya 3 katika fani husika. |
| | (Technician Certificate) NTA Level 5 | Cheti ya NTA level 4 kutoka chuo kinachotambuliwa<br>au<br>Pasi moja na subsidiary katika kidato cha sita |
| | (Ordinary Diploma) NTA Level 6 | Cheti cha NTA level 5 kutoka chuo chochote kinachotambuliwa<br>au<br>Pasi moja na subsidiary katika kidato cha sita ila mwombaji atalazimika kuanzia level 5 na hivyo kozi kuwa ya miaka 2 |
| Kilimo (General Agriculture) | (Basic Technician Certificate) NTA Level 4 | Ufaulu wa pasi ya D kwa masomo manne (4) ya kidato cha nne kati yake masomo hayo mawili (2) yawe ya sayansi yaani Biology, Chemistry, Physics au Engineering Science, Geography, Mathematics na Agriculture Science |
| | (Technician Certificate) NTA Level 5 | Cheti cha NTA Level 4 katika fani ya Kilimo kutoka chuo chochote kinachotambuliwa |
| | (Ordinary Diploma) NTA Level 6 | Cheti cha NTA level 5 katika fani ya Kilimo kutoka chuo chochote kinachotambuliwa |
| Certificate in Nursery teaching | Certificate (Two years) | Ufaulu wa pasi ya D kwa masomo mawili. |

## 5. MAMBO MUHIMU WAKATI WA USAJILI

Picha mbili (2) za rangi (passport) ulizopiga karibuni, Cheti cha kuzaliwa, Cheti cha kidato cha Nne/Sita/ au Tangazo la matokeo iwapo cheti hakijapatikana au Statement of Results. Kwa wanaohamia wanatakiwa kuleta nambari zao za Usajili kutoka chuo watokacho.

## 6. UTHIBITISHO WA AFYA

Mwanachuo/mwombaji atatakiwa kwenda kupimwa katika hospitali yeyote inayotambuliwa na Serikali, kwa kutumia fomu ya uthibitisho wa Daktari iliyoambatanishwa na fomu hii. Pia kila mwanachuo anatakiwa kuwa na Bima ya Afya itakayomsaidia kupata matibabu katika hospitali zilizopo jirani na chuo, walio na Bima za Afya wataendelea kutumia walizonazo.

**7. MAADILI YA CHUO**

Wanafunzi wanaosajiliwa Chuoni (STIMAT) watatarajia kufuata sheria, kanuni na taratibu za Chuo. Taratibu hizo ni pamoja na zile za Nidhamu (Disciplinary Bye-laws), Kanuni na Taratibu za Uendeshaji Mitihani (Regulations and Procedures for Administration of Examinations) na taratibu nyingine za uendeshaji wa shughuli mbalimbali za chuo kama zitakavyotolewa mara kwa mara na Mkuu wa Chuo. STIMAT haina sare rasmi isipokuwa kwa wanachuo wa kozi ya Kilimo – Makoti mawili marefu (overcoats) moja la kijani na jingine jeupe. Kwa wanafunzi wa Utunzaji wa Nyaraka, Kumbukumbu na Habari (Suti yaani koti na sketi au suruali ya rangi nyeusi). Wanachuo wa kozi zilizobakia wanatakiwa kuvaa nguo zenye staha na kuzingatia maadili mema.

**8. BWENI NA CHAKULA**

Chuo kina hosteli zenye umeme na maji ndani ya chuo. Pamoja na hosteli mwanachuo atakabidhiwa kitanda na godoro. Mwanachuo hatalipa gharama za umeme na maji kwani zimejumuishwa na gharama za hosteli. Gharama za Hosteli (malazi) ni kiasi cha shilingi 250,000.00 kwa mwaka ambazo hulipwa kwa awamu mbili za 125,000.00 kwa semesta. Chuo kina kantini (mgahawa) unaotoa huduma ya chakula kwa gharama ya Tsh 2000.00 kwamilo mitatu ya siku moja. Chuo pia kinaruhusu wanafunzi kupata chakula nje ya chuo au kwa kujiandalia wenyewe.

**9. VIFAA VYA KUJA NAVYO**

Kila mwanachuo tarajali anatakiwa kuja na vitu vifuatavyo:

(i) Rimu moja ya karatasi nyeupe (saizi ya A4) -itakabiidhiwa chuoni;
(ii) Blanketi 1 na shuka 2;
(iii) Chandarua ya pembenne;
(iv) Daftari kubwa 10;
(v) Ndoo ya plastiki;
(vi) Mahitaji binafsi kama sabuni, miswaki na vifaa binafsi vya usafi;
(vii) Nguo za michezo;
(viii) Mavazi binafsi ya kutosha zikiwamo za msimu wa baridi.

**10. MAHITAJI MAALUMU**

Wanachuo tarajali wa **kozi ya Kilimo** wanapaswa kuja na fedha ya ziada kwa ajili ya kununulia vifaa vifuatavyo ambavyo vinapatikana hapa Songea kwa urahisi:

(i) Buti za plastiki (Gum Boots) jozi moja;
(ii) Jembe la mkono lenye mpini;
(iii) Fyekeo na panga;

**11. SKOLASHIPU YA STIMAT KWA KAZI WA MANISPAA YA SONGEA**

Kwa wakazi wa Manispaa ya Songea, chuo kina utaratibu wa kutoa Skolashipu ambayo mwanafunzi aliyesoma Sekondari ya Kata katika Manispaa ya Songea atalipa nusu ya Karo/Ada ya Masomo. Skolashipu hii ya Mwenyekiti wa Bodi ya STIMAT inatolewa kwa walioamliza kidato cha nne ndani ya miaka miwili iliyopita.

**12. MUUNDO WA MALIPO**

Ada na michango mingine yote italipwa kabla ya usajili wa mwombaji kukamilika na utalipa **Akaunti Na. 0150245471600**, Jina la Akaunti *St. Thomas Institute of Management and Technology,* **CRDB Bank** kwa mchanganuo ufuatao:

| **GHARAMA ZA MWANACHUO WA BWENI** | | | | **GHARAMA ZA MWANACHUO WA KUTWA** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| MUHULA | AINA ZA MALIPO | KIASI | | MUHULA | AINA ZA MALIPO | KIASI |
| MUHULA WA KWANZA | Hosteli | 125,000.00 | | MUHULA WA KWANZA | | |
| | KARO/Ada ya Masomo | 370,000.00 | | | KARO/Ada ya Masomo | 370,000.00 |
| | Usajili | 30,000.00 | | | Usajili | 30,000.00 |
| | Ada za Mitihani (I) | 30,000.00 | | | Ada za Mitihani (I) | 30,000.00 |
| | Fedha za Tahadhari | 30,000.00 | | | Fedha za Tahadhari | 30,000.00 |
| | Serikali ya Wanafunzi (STIMATSO) | 5,000.00 | | | Serikali ya Wanafunzi (STIMATSO) | 5,000.00 |
| | Usajili wa Mwanachuo (NACTE) | 20,000.00 | | | Usajili wa Mwanachuo (NACTE) | 20,000.00 |
| | Kitambulisho cha Mwanachuo | 10,000.00 | | | Kitambulisho cha Mwanachuo | 10,000.00 |
| | Bima ya Afya (NHIF) kama unayo hutalipia | 54,000.00 | | | Bima ya Afya (NHIF) kama unayo hutalipia | 54,000.00 |
| | *Jumla ya Muhula wa Kwanza* | *674,000.00* | | | *Jumla ya Muhula wa Kwanza* | *549,000.00* |
| | | | | | | |
| MUHULA WA PILI | Karo/Ada za Masomo | 420,000.00 | | MUHULA WA PILI | Karo/Ada za Masomo | 420,000.00 |
| | Tozo ya Udhibiti Ubora (NACTE) | 15,000.00 | | | Tozo ya Udhibiti Ubora (NACTE) | 15,000.00 |
| | Ada za Mitihani (II) | 30,000.00 | | | Ada za Mitihani (II) | 30,000.00 |
| | Ada ya Cheti | 30,000.00 | | | Ada ya Cheti | 30,000.00 |
| | Gharama za Mahafali | 25,000.00 | | | Gharama za Mahafali | 25,000.00 |
| | Gharama za Mazoezi kwa Vitendo Kazini (Field Training) | 15,000.00 | | | Gharama za Mazoezi kwa Vitendo Kazini (Field Training) | 15,000.00 |
| | Hosteli | 125,000.00 | | | | |
| | | | | | | |
| | *Jumla ya Muhula wa Pili* | *660,000.00* | | | *Jumla ya Muhula wa Pili* | *535,000.00* |
| | Jumla Kuu | 1,334,000.00 | | | Jumla Kuu | 1,084,000.00 |

St. Thomas Institute of Management and Technology
(Songea Campus - Fully Accredited, Reg. No. NACTE/BTP/008; Msata Campus Reg. No. NACTE/BTP/092P)
Airport Road, Ruhuwiko, P. O. Box 998, SONGEA
Pugini area, Msata Township, P. O. Box 163, CHALINZE
chagua@stimat.ac.tz, www.stimat.ac.tz
Tel: 0767778069, 0622818818, 0765914576, 0717710468, 0763409901

# REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART A:**

**To the Medical Officer**
…………………………….

…………………………….

**From**: Principal,
St.Thomas Institute of Management &Technology (STIMAT),

Mr./Mrs./Miss (student)…………………………………………………………………….

Please examine the above named as to his/her fitness for undergoing the Certificate and/or Diploma Course in St. Thomas Institute of Management and Technology.

**…………………………..**
**Registrar - STIMAT**

**- - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - -**

## PART B:

## MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by Medical Officer)

I have examined the above and consider that he/she is physically fit/unfit to undergo the Certificate/Diploma Course stated above in Songea (Ruvuma Region).

Date ………………….....……….

Signature ……………………

Station ……………………..……….

Designation …………………

Official Stamp